

## **UENDELEZAJI WA KILIMO CHA KOROSHO**

### **1. Utangulizi**

Katika msimu wa 2017/18 Wilaya imezalisha miche 480,000 ya mikorosho kwa kushirikiana na bodi ya Korosho. Miche ya mikorosho imezalishwa na vikundi 7 vya Madizini SACCOS, Wilunze Korosho, Anacardium, Keneth, WARC Kibakwe, Good Hope na Gereza -Mpwapwa.

Vijiji ambavyo vipo kwenye mpango wa kuendeleza zao la korosho msimu wa 2017/18, Ni kama ifuatavyo: Ilolo, Mazae, Kisokwe, Idilo, Chunyu, Nghambi, Kazania, Berege, Chitemo, Sazima, Igoji I, Chinyika, Igoji II, Vinghawe, Kimagai, Inzomvu, Pwaga, Godegode, Kingiti, Lukole, Iyenge, Kibakwe na Ikuyu.

Shughuli za maandalizi ya mashamba na kuchimba mashimo zinaendelea katika vijiji 17.

### **JEDWALI LA MALENGO LA ZAO LA KOROSHO MSIMU 2017/18**

<b>NA</b>	<b>MBEGU ZILIZOPOKELEWA(KG)</b>	<b>MICHE ZALISHWA</b>	<b>IDADI YA WAKULIMA TARAJIWA KUPATA MICHE</b>	<b>JUMLA YA EKARI ZITAKAZO PANDWA</b>
1	5774	480,000	1,784	19,200

### **2. MIKAKATI YA UENDELEZAJI WA ZAO LA KOROSHO**

#### **Kuunda na Kuendeleza vikundi vya kuzalisha miche ya korosho**

Katika msimu wa kilimo 2017/18 jumla ya vikundi 7 vimeshiriki kwenye uzalishaji wa miche ya korosho.

#### **Uanzishaji wa mashamba darasa,**

Jumla ya mashamba darasa 17 yanatarajiwa kuanzishwa kwenye vijiji vinavoendeleza zao la korosho katika Sule na wakulima.

#### **Uhamasishaji wa upandaji wa korosho vijijini,**

Uhamasishaji wa upandaji wa korosho umefanyika katika kata 26, madiwani na wakuu wa Idara na taasi zilizopo kwenye ukanda wa chini ambapo mpaka sasa jumla ya wakulima 1,784 wameandikishwa kupanda korosho.

#### **Kuratibu usambazaji wa pembejeo za ruzuku,**

Katika msimu wa Kilimo 2017-18 Wilaya ilipokea kiasi cha Kilo 2000 za Sulpha, Movil lita 70 na Suba Chlo lita 200, Mupaphose lita 3 na RAV lita 2 ambapo jumla ya wakulima 203 wamegawiwa pembejeo. Hata hivyo halmashauri itaendelea kuandaa mahitaji ya

madawa pindi yanapohitajika, na kuomba bodi ya korosho kuwezesha wakulima kupitia ruzuku.

### **Usambazaji wa miche ya korosho**

Katika vijiji 17 vinavyoendeleza zao la Korosho, Usambazaji wa miche ya korosho inatarajiwa kufanyika mwezi Disemba mara baada ya mvua kunyesha.

### **Kufanya kikao cha wadau wa Korosho Cha Wilaya**

Ili kuendeleza Kilimo cha Korosho Kikao cha wadau wa Korosho kinatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi Disemba 2018

### **Kukuza ubanguaji mdogo na wa kati**

Ununuzi wa mashine moja ya ubanguaji wa Korosho umeingizwa Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 kupitia mapato y ndani.

### **Kukuza masoko ya ndani ya zao la korosho**

Katika msimu wa Kilimo 2016/17 Jumla ya kilo 3,556 zimeuzwa kwa kampuni ya Mohamed Enterprises Ltd ya nchini Tanzania. Kiasi hicho ni kidogo, Hivyo wakulima wanashuriwa kuongeza upandaji na uzalishaji zaidi ili wafanya biashara wawe na uhakika na wingi wa korosho pindi wanapohitaji. Kwa sasa korosho zote zinauzwa kupitia vyama vya ushirika (STAKABADHI GHALANI), Halmashauri imeomba LIC kuwezesha uundwaji wa chama cha ushirika.

### **Kutoa elimu kwa wakulima namaafisa ugani**

Elimu ya Kilimo cha korosho inaendelea kutolewa kwa wadau mbalimbali kupitia maafisa ugani wote, hata Hivyo Halmashauri imeomba fedha kutoka LIC ili kuwezesha utoaji elimu kwa wingi, kwani imeonekana kuwa bado maafisa ugani na wakulima wengi wanahitaji elimu zaidi ya zao hilo.

**Mohamed A. Maje**  
**MKURUGENZIMTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YAMPWAPWA**